

MKATABA WA UPANGAJI

Mkataba huu umefanyika leo tarehe 01- Mwezi 03 Mwaka 2025

BAINA YA

HELLEN WILLIAM URONU wa Mbwen, Manispaa ya Kinondoni ,mkoa wa Dar Es Salaam (ambaye ataitwa **MPANGISHAJI**), ambapo kanuni na masharti ya mkataba huu yatawahusisha warithi wake, wasimamizi wake wa kisheria kwa upande wa kwanza.

NA

EIST TECHNOLOGY COMPANY LIMITED wa S. L. P 42797 Dar Es Salaam (ambaye anaitwa **MPANGAJI**), ambapo kanuni na masharti ya mkataba huu yatawahusisha warithi wake, wasimamizi wake wa kisheria kwa upande wa pili.

A. KWA KUWA,

Mpangishaji ni mamiliki halali wa lililopo Boko-Dovya, Manispaa ya Kinondoni, Mkoa wa Dar Es Salaam, kwa Mkataba huu ameamua kumpangisha Mpangaji eneo hilo kwa ajili ya shughuli za kiofisi.

B. KWA KUWA,

Mpangishaji amethibitisha kuwa yeye yupo kwenye umiliki halali wa kisheria wa eneo tajwa hapo juu na kwamba yupo tayari kwa hiari yake mwenyewe kupangisha eneo tajwa hapo juu.

C. NA KWA KUWA

Mpangaji kwa hiari yake mwenyewe ameamua kupanga sehemu tajwa kwa lengo la shughuli za kiofisi, kwa masharti na makubaliano kama yanavyoonekana kwenye mkataba huu;

NA, HIVYO BASI Mkataba huu unashuhudia yafuatayo:-

1. Kwamba, Mpangishaji anampangishia Mpangaji eneo tajwa hapo juu kwa kipindi cha miezi sita kuanzia tarehe 01 Mwezi wa 03 mwaka 2025 na kuishia tarehe 30 Mwezi 09 Mwaka 2025
2. Kwamba, Kodi ya sehemu hiyo itakuwa Shilingi za Kitanzania Laki tano (Tshs 500,000. /) tu kwa kila mwezi Mmoja.
3. Kwamba fedha tajwa hapo juu zitalipwa kama fedha taslimu kwa Mpangishaji
4. Kwamba Mpangishaji anampangisha Mpangaji sehemu tajwa hapo juu kwa ajili ya shughuli za kiofisi na kiwanda na sio kwa ajili ya kazi nyingine.

5. Kwamba, Mpangaji hatakiwi kumpa mtu mwingine sehemu tajwa kwa matumizi ya namna yoyote.
6. Kwamba, mkataba huu utavunjika wenyewe moja kwa moja endapo mpangaji akishindwa kulipa kodi ya pango kwa wakati.
7. Kwamba, mkataba huu unaweza kuvunjwa kwa maridhiano ya pande zote mbili endapo kutakuwa na mabadiliko ya lazima katika mkataba huu
8. Kwamba, Mpangaji anatakiwa kutoa taarifa mapema ya mwezi mmoja (1) kabla ya mkataba huu kumalizika kama ataendelea kupanga na yuko tayari kusaini mkataba mwingine.
9. Kwamba, Mpangaji kama atataka kuendelea kupanga katika eneo hilo baada ya mkataba huu kuisha muda wake basi atalipa malipo ya pango jipya mwezi mmoja kabla ya kodi ya pango la zamani kuisha/ kumalizika
10. Kwamba, mpangaji atatakiwa kutoa taarifa ya miezi mitatu (3) kabla, kama atataka kufanya mabadiliko yoyote ya kimkataba kama vile kuvunja mkataba au kusambaratisha au kugawa kwa pande zote mbili.
11. Kwamba, Mpangishaji atakuwa na uwezo wa kupanga bei upya au kubadili masharti ya mkataba kila mkataba mpya unaposainiwa.
12. Kwamba, Mpangaji haruhusiwi kupangisha mtu mwingine bila idhini ya Mpangishaji.
13. Kwamba mkataba huu ni lazima ulindwe na kuheshimiwa na pande zote mbili, na atakayevunja mkataba huu kati ya pande hizi mbili atapoteza haki zake zote

KWA KUSHUHUDIA HAYA pande zote mbili zimeweka sahihi zao hapa chini katika tarehe zinazoonekana hapa.

IMESAINIWA na KUTOLEWA hapa Dar es Salaam na
HELLEN WILLIAM URONU ambaye
ambaye ninamfahamu/ Ametambulishwa kwangu na

.....
leo tarehe 10..... mwezi 03....., 2025

.....
MPANGISHAJI

MBELE YANGU

JINA: JOHN J. LINGGOLA

SAHIHI: 

2 | Page




ANUANI: 31909 DSM
WADHIFA: WAKILI

IMESAINIWA na KUTOLEWA hapa Dar es Salaam na
EIST TECHNOLOGY COMPANY LIMITED ambaye
ambaye ninamfahamu/ Ametambulishwa kwangu na
.....
leo tarehe 10..... mwezi ... 03....., 2025


.....
MPANGAJI

MBELE YANGU

JINA: JOHN J. LINGOLA
SAHIHI: 
ANUANI: 31909 DSM
WADHIFA: WAKILI

